KAMISHNA Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (katikati) akiwa na Mkuu wa Uhamiaji wa Rwanda, Lynder Nkuranga (kulia) na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)Alphayo Kidata. (Picha na Uhamiaji).

Zanzibar na kilo moja inayopimwa hapa Bara iwe sawa. Kwa viongozi hawa kuja hapa ushirikiano unazidi kuimarika na tutaongea lugha moja," alisema.

UHURU UK 4.

# Kamati ya Bunge yaridhishwa ujenzi kiwanda cha nyama

**Morogoro**
**NA LATIFA GANZEL**

KAMATI ya kudumu ya Bunge, Uwezeshaji Mitaji kwa Umma (PIC) imeridhishwa na uwekezaji uliofanywa katika kiwanda cha nyama cha Nguru Hills Estate, kilichopo wilayani Mvomero.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jerry Slaa aliyasema hayo jana baada ya kamati hiyo kutembelea kiwanda hicho kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea kufanywa za ujenzi ambapo kinatarajiwa kuanza hivi karibuni.

"Fedha zilizowekwa na serikali kupitia mfuko wa PSSSF zinaonekana thamani yake, fedha zilizowekezwa zitarudi baada ya muda mfupi," alisema.

Alisema kiasi cha dola milioni 15 zilizotumika katika kiwanda hicho zimewekezwa kwenye tija na kiwanda hicho kitakuwa cha mfano nchini.

Aidha, alisema uwekezaji huo utakapokamilika utasaidia walaji wa nyama na upatikanaji wa ngozi zenye ubora nchini pamoja na wafugaji kuweza kuuza mifugo yao katika soko la uhakika.

Mwenyekiti huyo aliagiza Bodi ya Wadhamini ya PSSSF kuhakikisha inaendelea kusimamia mkataba wa uwekezaji kwa kushirikiana na wabia wenzake kwa lengo la kuhakikisha uzalishaji unaanza haraka ili kupata tija.

Pia, kamati hiyo iliagiza Bodi ya PSSSF kuongeza kipengele katika makubaliano yao na wewekezaji wenza ambao ni kiwanda cha Nguru Hills Limited kiuze ngozi katika kiwanda cha ngozi Kilimanjaro ambacho PSSSF imewekeza ili kipate malighafi za kuendesha.

Vilevile, iliagiza PSSSF na wawekezaji wenza kuanzisha programu maalum kwa wafugaji ili kuwa na mifumo maalumu itakayokidhi kupata viwango vya mifugo vinavyokubalika katika kiwanda hicho.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku ambapo kinatarajia kuanza rasmi muda wowote mwaka huu.

Alisema mradi huo wa machinjio hayo ya kisasa unamilikiwa kwa ubia na wanahisa watatu kati ya serikali kupitia mfuko wa PSSSF, Eclipse Investiment (LLC) na kampuni ya Busara Investiment (LLP)

Alibainisha kuwa mradi huo ulianza mwaka 2018 lakini ugonjwa wa Uviko-19 ulipoanza ulisababisha mashine zilizoagizwa kutoka nje kuchelewa kuletwa wakiwemo na wataalamu wake hadi kufikia Julai mwaka jana.

Scanned with CamScanner

kutatua tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa kwenye shule hiyo kuondoa msongamano kwa wanafunzi.

(kulia), alipokitembelea mkoani humo, jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

NIPASHE UK 7.

# Uwekezaji machinjio ya kisasa walikuna Bunge

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, imeridhishwa na uwekezaji unaoendelea wa mradi wa fedha za serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mashirika ya Umma (PSSSF) kwenye Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch Limited kilichoko Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alitoa kauli hiyo baada ya kamati hiyo kutembelea kiwanda hicho na kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea kufanywa za ujenzi wake ambao kinatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Silaa alisema kamati hiyo imeridhishwa baada ya kuona fedha zilizowekwa na serikali kupitia PSSSF zinaonekana thamani yake na kuna matumaini makubwa fedha zilizowekezwa zitarudi baada ya muda mfupi.

Alisema Kamati imejionea bila shaka kuwa fedha zilizowekezwa Dola milioni 15 kwenye kiwanda kikubwa cha kisasa cha nyama zimewekezwa kwenye tija na kiwanda kitakachokuwa cha mfano nchini.

"Kamati ya Bunge imeridhishwa kwa uwekezaji huu utakapokamilika utasaidia walaji wa nyama na upatikanaji wa ngozi zenye ubora nchini," alisema Silaa.

Hata hivyo, aliiagiza Bodi ya Udhamini ya PSSSF kuhakikisha inaendelea kusimamia mkataba wa uwekezaji kwa kushirikiana na wabia wenzake, kwa lengo la kuhakikisha uzalishaji unaanza haraka ili kupata tija.

Agizo lingine kwa PSSSF ni kuongeza kipengele katika makubaliano yao na mwekezaji mwenza ambao ni Kiwanda cha Nguru Hills Limited kiwauzie ngozi Kiwanda cha Ngozi cha Kilimanjaro ambacho PSSSF imewekeza ili kipate malighafi za kuendesha.

Agizo lingine ni PSSSF na wawekezaji wenza kuanzisha programu maalum kwa wafugaji ili kuwe na mifumo maalum itakayokidhi kupata viwango vya mifugo vinavyokubalika katika kiwanda hicho.

Awali akitoa taarifa kwa kamati hiyo kuhusu Kiwanda cha Machinjio ya kisasa, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Alisema mradi huo wa machinjio hayo ya kisasa yanamilikiwa kwa ubia wa wanahisa watatu kati ya serikali kupitia PSSSF, Eclipse Investment (LLC) na Kampuni ya Busara Investment (LLP).

Scanned with CamScanner